# Mradi wa Uimarishaji wa Huduma Muhimu za Afya (MUHUMA)

*(Mradi wa pamoja kati ya Wizara ya Afya na Shirika la Kimataifa la Maendeleo na Utafiti la Canada (IDRC)*

## Muhtasari Na.1: Mapitio ya MUHUMA



*MUHUMA imeandaa miundombinu kadhaa ambayo inazisaidia menejimenti za afya kwenye wilaya katika ukusanyaji na kuratibu taarifa.*



Rasilmali kwa ajili ya utoaji wa afya ya msingi kwa wananchi kwenye nchi zinazoendelea ni tatizo kubwa. Mwaka1993, Ripoti ya Mkakati wa Maendeleo Duniani ilihimiza uwekezaji wa rasilimali ya kutosha katika sekta ya afya. Ripoti hiyo pia ilihimiza matumizi ya rasilimali kidogo iliyopo katika kutatua matatizo makubwa ya kiafya. Ripoti hiyo pia ilishauri kuwa utoaji wa huduma bora ya afya pamoja na vitendea kazi kwa asilimia 80 ya wananchi kwenye nchi ambazo zina kipato cha chini sana kunaweza kupunguza matatizo ya magonjwa sugu na yanayojitokeza mara kwa mara.

Tangu mwaka 1997 Mradi wa Uimarishaji wa Huduma Muhimu za Afya (MUHUMA) umekuwa ukifanya juhudi za kutekeleza utoaji wa huduma bora za afya ikiwa ni pamoja na uimarishaji wa menejimenti za afya katika wilaya mbili za Tanzania - Rufiji na Morogoro.
MUHUMA imekuwa ikitafiti mbinu za kuboresha mfumo wote wa huduma ya afya katika ngazi ya wilaya. Katika zoezi hilo uimamrishaji wa menejimenti za afya katika wilaya umetiliwa mkazo sana kwa kuwashirikisha wadau wote. Kutokana na kuhusisha utafiti na juhudi za kutafuta maendeleo, MUHUMA imeweza kubuni njia za utendaji na ukusanyaji habari ambazo zimeziwezesha menejimenti za afya katika ngazi ya wilaya kuweza kutengeneza mipango yao wenyewe. Menejimenti hizi zinaweza sasa kutumia takwimu ambazo zinapatikana huko huko wilayani katika kupanga mipango yao na kutafuta mbinu za utekelezaji badala ya kusubiri kuletewa mipango hiyo kutoka ngazi za juu. Kwa hatua hiyo, utoaji wa huduma ya afya sasa unalenga katika maeneo ambayo yana matatizo makubwa ya afya.

MUHUMA,mradi unaoendeshwa kwa pamoja kati ya Shirika la Maendeleo na Utafiti la Canada (IDRC) na Wizara ya Afya katika kutekeleza mradi huu umekusanya nguvu za pamoja za kitaifa na kimataifa. Mradi huu unachangia katika utekelezaji wa mabadiliko ya Sera ya Afya nchini ambayo ina lengo la kuboresha ufanisi na upatikanaji wa huduma bora ya afya katika nchi nzima.

**Jinsi MUHUMA inavyofanya kazi**

MUHUMA iko msitari wa mbele katika kuchochea ushirikishwaji wa wananchi katika kupanga mipango yao ya maendeleo na kuweka kipaumbele hususan katika sekta ya afya na hatimaye kupima matokeo baada ya utekelezaji. Mradi unatekeleza haya kwa:-

***Kusaidia utafiti:*** MUHUMA ina mpango wa utafiti katika maeneo manne: Kuunda na kuendeleza mipango ya wilaya; kuweka kumbukumbu ya mabadiliko katika utaratibu wa huduma za afya kwenye menejimenti ya afya katika halmashauri za wilaya na sehemu za utoaji wa huduma za afya ngazi zote.

Pia mradi huu unafuatilia matokeo ya huduma za afya kwa wananchi kuanzia ngazi ya familia. Watafiti katika mradi huu wamechukuliwa kutoka taasisi mbalimbali hapa nchini.

***Kusaidia maendeleo:*** MUHUMA inasaidiana na wadau wengine katika kuandaa miundo mbinu ambayo inaziongezea uwezo menejimenti za afya kwenye halmashauri za wilaya katika kupanga mipango na kuiendesha kwa kutumia rasilimali zilizoko vijijini. Mradi pia unazisaidia menejimenti za afya za wilaya kutumia mbinu walizojipangia wananchi wenyewe katika kutekeleza mipango hiyo.

***Utoaji wa fedha:*** Ili kuziwezesha menejimenti za afya kuweza kutekeleza mipango yake, mradi umeongeza bajeti kwa takribani dola ya Kimarekani moja kwa kila mtu kwa mwaka. Kutokana na ongezeko hilo ambalo linazigusa wilaya zote mbili, bajeti ya afya imefikia takriban dola za Kimarekani nne kwa kila mtu kwa mwaka. Kwa ujumla, mipango ya huduma ya afya, utoaji wa huduma yenyewe na matumizi ya huduma ya afya yameongezeka na kuboreka. Hivi sasa, Kitengo cha Utafiti cha Mradi kinapima matokeo ya uboreshaji wa huduma hiyo. Tanzania hivi sasa imeanzisha mpango wa uchangiaji huduma za afya kwa karibu theluthi mbili katika wilaya zote chini ya mradi wa serikali wa kuichangia huduma ya afya ambao unaendeshwa kwa pamoja na wahisani.

**Mbinu za mipango ya afya**

MUHUMA imeandaa miundo mbinu kadha ambayo inazisaidia menejimenti za afya kwenye wilaya katika ukusanyaji na kuratibu taarifa. Mbinu hizo ni pamoja na:-

***Tathmini ya Magonjwa*** ambayo yanajitokeza zaidi katika jamii na mahitaji ya tiba:

***Mahesabu ya Huduma za Afya*** katika ngazi ya wilaya ambayo yanaonyesha makisio na matumizi kulingana na magonjwa yaliyopo kwa viwango mbalimbali.

***Utaratibu wa Utoaji wa Taarifa*** ambao unonyesha udhaifu katika utoaji wa huduma bora na pale ambapo gharama ni kubwa.

***Sauti ya Wananchi*** ambao inahimiza ushirikishwaji wa jamii katika kupanga na kutekeleza mipango ya huduma ya afya na hivyo kuiboresha.

Miundo mbinu hii inasaidia kuziwezesha menejimenti za afya za halmashauri kutengeneza mipango muafaka inayopewa kipaumbele katika kutenga rasilimali na utekelezaji wake.

Kwa mfano, kwa kutumia miundo mbinu iliyosimamiwa na MUHUMA, mameneja wa mipango ya afya wanafanya kila jitihada ya kutenga fedha za kutosha ili kupambana na magonjwa ambayo yanawasumbua zaidi wananchi katika wilaya. Tafiti zilizofanywa zimeoneysha kwamba ugonjwa wa malaria unasababisha vifo kwa asilimia 30. Matokeo yake ni kwamba menejimenti za afya za halmashauri za wilaya katika mipango yake zimeongeza matumizi kwa ajili ya kupambana na ugonjwa huu kutoka asilimia 5 hadi 25.

**Washiriki**

Washiriki wa MUHUMA wanafanya kazi pamoja na Kamati ya Kitaifa ya Afya hususan katika kutoa miongozo ya sera katika kuendeleza kutekeleza miradi. Wanaoshirikiana na MUHUMA ni: Serikali ya Tanzania (Wizara ya Afya na Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa), Shirika la Maendeleo na Utafiti la Canada (IDRC), Shirika la Afya Duniani (WHO), Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Watoto na Elimu (UNICEF), Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Canada (CIDA).

Washiriki katika utekelezaji wa mradi ni pamoja na Kituocha Utafiti na Maendeleo cha Ifakara, Chuo Kikuu cha Afya ya Jamii, Taasisi ya Afya ya Jamii na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Taasisi ya Maendeleo ya Mihula.

MUHUMA inawahudumia zaidi ya watumishi 70 katika utafiti na tathmini pamoja na wengine 10 ambao wanafanya kazi kwa vipindi maalum katika utafiti. Timu ya watekelezaji wa mradi huu wapo kwenye ofisi za Taasisi ya Uchunguzi wa Magonjwa (NIMR) mjini Dar es Salaam, Tanzania.

**Kwa habari zaidi wasiliana na:**

**Mradi wa Uimarishaji wa Huduma Muhimu za Afya (MUHUMA),**
**Sanduku la Posta 78487,**
**Dar es Salaam, Tanzania**
**Simu: (255) (022) 213 0627**
**Fax: (255) (022) 211 2068**
**Barua Pepe: info@tehip.or.tz**

Shirika la Kimataifa la Maendeleo na Utafiti la Canada (IDRC) ni shirika la umma ambalo limeundwa kwa mujibu wa Sheria ya Bunge la Canada ya mwaka 1970. Madhumuni yake ni kuwasaidia watafiti na jamii kwa ujumla katika maendeleo ya dunia na kutafuta ufumbuzi wa matatizo ya kijamii, kiuchumi na mazingira. Msaada pia unatolewa katika kuendeleza tafiti kwa wazawa na kujenga uwezo katika kuunda sera zinazoendana na matumizi ya teknolojia mpya katika nchi zinazoendelea ili kujenga jamii yenye afya bora, na yenye usawa na ustawi.